

Jilinde Mwenyewe Kifedha

<https://www.consumerfinance.gov/about-us/blog/protect-yourself-financially-from-impact-of-coronavirus/>

Msaada wa Rehani kwa Wakazi wa Washington

- Ikiwa huwezi kulipa mkopo wako wa nyumba (rehani), au unaweza kulipa kiasi tu cha mkopo, wasiliana na msimamizi wako wa mkopo mara moja.
- **Ushauri na msaada wa Umiliki wa Nyumba vinapatikana kwa wakazi wa Washington**, bila kujali nani anayemiliki au anayehudumia mkopo. Wamiliki wa Nyumba wanaweza kupiga simu kwa namba ya bure ya DFI **1-877-RING-DFI (746-4334)** ili kupata msaada wa kuwasiliana na msimamizi wao wa rehani, na kujua zaidi kuhusu machaguo. Kufanya kazi na mshauri wa makazi, piga simu kwa Namba ya Simu ya Umiliki wa Nyumba ya Washington kwa **1.877.894.HOME (4663)**. Huduma ya mkalimani inapatikana kwenye namba zote mbili.

Sheria ya Msaada, Unafuu, na Ulinzi wa Uchumi Wakati wa Virusi vya Korona (CARES)

imeweka kinga mbili kwa wamiliki wa nyumba kwa mkopo wa nyumba uliofadhiwa na serikali kuu.:

1. Mkopeshajiv au msimamizi wako wa mkopo hawezi kuweka zuio hadi baada ya Des. 31, 2020 - tembelea www.hud.gov kwa taarifa mpya. Hasa, Sheria ya CARES inawakataza wakopeshaji na wasimamizi wa mkopo kuweka zuio la mahakama au lisilo la mahakama dhidi yako, au kukamilisha hukumu ya kuweka zuio au mauzo, kwa wakati huu. (**Zuio** ni mchakato wa kisheria ambapo mkopeshaji unachukua udhibiti wa mali, kumfukuza mmiliki wa nyumba na kuiuza nyumba baada ya mmiliki wa nyumba kushindwa kukamilisha malipo yote.)
2. Ikiwa unakabiliwa na tatizo la kifedha kwa sababu ya janga la virusi vya korona, una haki ya kuomba uvumilivu wa hadi siku 180. Pia una haki ya kuomba kuongezewa muda mwingine wa hadi siku 180. Lazima uwasiliane na msimamizi wako wa mkopo kwa ajili ya kuomba uvumilivu huu. Hakutakuwa na ada ya ziada, adhabu au riba ya ziada (zaidi ya kiasi kilichopangwa) kilichoongezwa kwenye akaunti yako. **Uvumilivu** ni pale msimamizi wako wa rehani, kampuni ambayo inatuma maelezo ya mkopo na inayosimamia mkopo wako, au mkopeshaji anapokuruhusu upumzike kulipa au kupunguza malipo yako kwa muda mfupi. Uvumilivu wa mkopo haufuti kile unachodaiwa. Utapaswa kulipa malipo yoyote ambayo hayajalipwa au yaliyopunguzwa hapo baadae.

Utapeli

Utapeli wa Uwekezaji Wakati wa COVID-19: Kabla ya kufanya maamuzi yoyote makubwa ya uwekezaji, wawekezaji wanapaswa kufanya utafiti na kuthibitisha kwamba wanafanya kazi na wataalam wa fedha wenye kibali. Piga simu 877-RING-DFI (746-4334) kwa msaada.

Vidokezo vya Kuepuka Udanganyifu

- Mashirika ya serikali hayatakupigia simu wala kukutumia ujumbe kuhusu mafao au fedha, na hayatakuomba kuweka amana, ada, au malipo mengine ili kupata mafao yako.
- Mashirika ya serikali hayatakuomba namba yako ya Hifadhi ya Jamii, namba ya akaunti ya benki, au namba ya kadi ya mkopo.
- Chukua tahadhali ya barua pepe, simu, na jumbe kutoka vyanzo ambavyo huvijui.



WA Dept. of Financial Institutions Msaada & Taarifa za Kifedha kwa Walaji Wakati wa COVID-19

Virusi vya Korona: Taarifa ya Wakopaji wa Mkopo wa Mwanafunzi

Kwa msaada wa mikopo yako ya wanafunzi, wasiliana na **Watetezi wa Mkopo wa Mwanafunzi wa Washington** kupitia Washington Student Achievement Council kwa loanadvocate@wsac.wa.gov au wapigie simu DFI kwa 877—746-4334 ili kuzungumza na mshirika wa timu yetu ya msimamizi wa mkopo wa elimu ya mwanafunzi.